

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MASASI

(Barua zote zielekezwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Simu:023 - 2510031

Fax: 023- 2510031

E-Mail: [ded-masasi@gmail.com](mailto:ded-masasi@gmail.com)

[Planning\\_masasi@gmail.com](mailto:Planning_masasi@gmail.com)



S.L.P. 60,

MASASI,  
MTWARA,  
TANZANIA

Kumb. Na MDC/B.10/1/V0L.IV

22/08/2017.

## **MPANGO KAZI WA MANUNUZI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2017-2018** **1.0 UTANGULIZI:**

Halmashauri ya Wilaya Masasi kama Taasisi Nunuzi (Procuring Entity) Inapaswa kuandaa Mpango Kazi wa Manunuzi wa Mwaka ,kila Mwaka wa Fedha Unapoingia kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 7 ya mwaka 2011 Kifungu Na. 49 na Kanuni Na. 69 -70 ya Manunuzi ya Umma G.N 446 ya mwaka 2013.

Mpango Kazi wa Manunuzi umeandaliwa kwa kuzingatia MTEF kwa mwaka wa 2017/2018 ambao ulipitishwa na vikao halali vya Kamati tatu za kudumu ikiwemo na Kamati ya Fedha Utawala na Mipango (FUM) na Mwisho Baraza la Madiwani la Halmashauri (W) Masasi. Mpango Kazi huu wa Manunuzi umeandaliwa kwa ushirikiano wa pamoja kati ya Idara na Vitengo Katika Halmashauri.

Aidha Mpango kazi huu wa Manunuzi umeandaliwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali ya Manunuzi kama ifuatavyo:-

1. Sababu za Kiuchumi na Kuleta ufanisi katika utekelezaji wa Mchakato Mzima wa Manunuzi kama vile Ununuzi wa Vifaa na Huduma Mtambuka ikiwemo shughuri za Ujenzi
2. Kuendeleza Fursa ya ushindani katika Ununuzi wa Vifaa na Huduma Mtambuka ikiwemo shughuri za Ujenzi na Kazi za Mtaalam Mshauri
3. Kuwawezesha Wazalishaji, Wakandarasi na Watoa Huduma wa Ndani Kushiriki kikamilifu katika kuomba na Kufanya Zabuni mbalimbali.
4. Kujenga Uadilifu, Uwazi,na Uwajibikaji na Usawa katika Mchakato Mzima wa Manunuzi.

## **2.0. MCHAKATO WA KUANDAA MPANGO KAZI WA MANUNUZI 2017/2018**

Ili kuwezesha Utekelezaji wa Kazi za Manunuzi, Manunuzi yote yakiwemo Ununuzi wa Vifaa, Huduma Mtambuka, Ujenzi na Huduma mbalimbali zilizoonyeshwa kwenye MTEF zimeingizwa ndani ya Mpango Kazi huu. Manunuzi haya yatatekelezwa kwa vyanzo vilivyotengwa katika Fedha za matumizi ya kawaida (OC) na Matumizi ya fedha za shughuli za Maendeleo na uendeshaji wa ofisi katika shughuri za kila siku. Kama inavyojionyesha katika jedwali hapo chini:-

S/N	CATEGORY	SYMBOL
(a)	Goods	G
(b)	Works	W
(c)	Non-Consultancy services	S
(d)	Consultancy Services	C

Orodha ya Vifaa, Huduma Mtambuka, Ujenzi na Kazi za Mtaalam mshauri zimeainishwa na kuwekwa katika fungate (package) kuliangana na aina, chanzo cha fedha na kiasi kilichotengwa. Kila Fungate imepewa njia ya Manunuzi ambayo Halmashauri kama taasisi nunuzi itatumika wakati wa mchakato wa kufanya Manunuzi.

### MUHTASARI WA KAZI ZA MANUNUZI 2017/2018

Halmashauri ya Wilaya ya Masasi katika Mwaka wa 2017/2018 inatarajia kutumia sh. **7,673,857,663.00** katika Manunuzi mbalimbali kama inavyosomeka hapo chini:-

S/N	Aina ya Manunuzi	Matumizi ya kawaida	Maendeleo	Jumla	%
1	Vifaa (G)	98,875,170.00	1,284,901,511.00	1,383,776,681.00	18.03
2	Huduma (S)	375,938,472.00	1,253,172,860.00	1,629,111,332.00	21.23
3	Ujenzi (W)	15,000,000.00	4,645,969,650.00	4,660,969,650.00	60.74
	JUMLA KUU	489,813,642.00	7,184,044,021.00	<b>7,673,857,663.00</b>	100

### 3.0 VIWANGO VYA NJIA ZA MANUNUZI:

Njia za Manunuzi zitakazotumika zimetajwa ukomo wa viwango vya matumizi ya njia hizo katika jedwali Na. 2 la Kanuni kama ifuatavyo:-

S/N	NJIA YA MANUNUZI	VIFAA	UJENZI	HUDUMA MTAMBUKA
1	International Competitive Bidding (ICB)	No limit	No limit	No limit
2	National Competitive Bidding (NCB)	Up to T.shs 1,000,000,000	Up to T. shs 5,000,000,000	Up to T.shs 1,000,000,000
3	Restrictive Tendering	No limit	No limit	No limit
4	Competitive Quotations/ National Shopping (NS)	Up to T.shs 120,000,000	Up to T.shs 200,000,000	Up to T.shs 100,000,000
5	Single Sourcing Procurement (SS)	No limit	No limit	No limit
6	Minor Procurement- minor value	Up to T.shs 10,000,000	Up to T.shs 20,000,000	Up to T.shs 10,000,000
7	Micro Value Procurement	Up to T.shs 5,000,000	Not applicable	Not applicable

#### 4.0 AINA ZINGINE ZA MANUNUZI

Kwa kuzingatia Kanuni Na. 130 ya Manunuzi G.N 446 ya mwaka 2013 Ununuzi wa vifaa na huduma Mtambuka unaweza kufanywa kupitia

1. GPSA au Wazabuni walioteuliwa na GPSA (Short Listed Suppliers)
2. Matengenezo ya Magari na Mitambo yatafanywa kupitia gereji zilizohitishwa na Mkurugenzi wa Tanzania Electrical and Mechanical Service Agency (TEMESA) wa Wizara ya Miundombinu kama ilivyoainishwa katika Kanuni 136 na 137 au authorized dealers aliyethitishwa kufanya Matengenezo ya Gari au Mtambo husika.
3. Ununuzi wa Dawa,Vifaa tiba,Vitendanishi vya maabara na Vifaa vya hospital utaratibu utakaotumika ni ule ulioainishwa katika kanuni nambari 139 inayotaka kununua mahitaji haya kutoka Msd

#### 4.1 VIWANGO VYA GHARAMA VYA MADARAJA KWA KAZI ZA UJENZI (PROCUREMENT OF WORKS)

(Class Limits for Building, Civil, Mechanical, Electrical and Specialist)

	CLASS LIMIT FOR ANY SINGLE CONTRACTOR(In million Tshs)
--	--

CLASS	CIVIL	BUILDING	MECHANICAL	ELECTRICAL	SPECIALIST
ONE	UNLIMITED	UNLIMITED	UNLIMITED	UNLIMITED	UNLIMITED
TWO	5,000	3,000	2,000	2,000	400
THREE	3,000	2,200	1,200	1,200	150
FOUR	1,500	1,200	600	600	-
FIVE	750	600	300	300	-
SIX	300	200	150	150	-
SEVEN	150	120	75	75	-

#### **4.2 KAZI ZA WATAALAM WASHAURI (PROCUREMENT OF CONSULTANCY SERVICES)**

Kwa kuzingatia jedwali Na. 2 Viwango vifuatavyo vitatumika kwa Zabuni za kazi zitazohitaji usimamizi wa Mtaalam Mshauri

S/N	NJIA YA MANUNUZI	KIWANGO
1	International Competitive Selection	No limit
2	National Competitive Selection	Up to Tshs.1,500,000,000
3	Restricted Competitive Selection	No Limit
4	Single –source selection	No limit
5	Individual Selection	Up to Tshs.150,000,000
6	Minol Value Procurement	Up to Tshs.10,000,000

Pamoja na maelezo tajwa hapo juu Mpango Kazi wa Manunuzi kwa Mwaka 2017/2018 umeambatanishwa.

Nawasilisha,

Henry Mushi,  
**Kny Mkurugenzi Mtendaji,**  
**Halmashauri (W) Masasi.**